

# Ripoti ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (SAM)

## Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

### Halmashauri ya Wilaya ya Magu

### Mkoa wa Mwanza

Sikika

2019

**Kwa Ufadhili wa Shirika la Maendeleo:**
**(With core support by DANIDA)**

ROYAL DANISH
EMBASSY
*Danida*

**Maelezo ya picha kutoka ukurasa wa kwanza:** Wajumbe wa timu ya SAM, wilayani Magu wakikagua shimo la kutupia kondo la nyuma la uzazi katika kituo cha afya Nyanguge wakati wa zoezi la uhakiki vituoni. Wapili kutoka kulia ni Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Omary Ramadhani.

Sikika

# Ripoti ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (SAM)

## Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

## Halmashauri ya Wilaya ya Magu

## Mkoa wa Mwanza

**Zoezi la SAM limetekelezwa na Sikika kwa Hisani ya Mradi wa IMPACT unaofadhiliwa na:**

**(SAM exercise was implemented by Sikika through specific support from IMPACT Project on behalf of)**

Canada

**Aprili 2019**

# Shukrani

Timu ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (SAM) ya wilaya ya Magu inathamini mchango wa kila mmoja aliyeshiriki katika utekelezaji wa zoezi la ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii kwa namna moja ama nyingine. Shukrani za dhati tunazitoa kwa taasisi za Aga Khan na Sikika kwa kuendesha mradi huu wenye lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi, baba mama na mtoto.

Vilevile timu inatoa shukrani kwa mamlaka zote za halmashauri ya Wilaya ya Magu tukianza na Mh. Dkt Philemon Sengati (Mkuu wa Wilaya), Lutengano G. Mwalwiba (Mkurugenzi Mtendaji), Dkt Maduhu Nindwa (Mganga Mkuu wa Wilaya), Hilal Elisha (M/kiti wa halmashauri), madiwani hususani wajumbe wa kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji), kamati ya uendeshaji ya huduma za afya ya halmashauri (CHMT), timu ya uendeshaji wa halmashauri (CMT), waganga wote wa vituo na wadau wote walioshirikiana na timu kukamilisha zoezi la SAM.

Mwisho, nawashukuru wajumbe wote wa timu ya SAM kwa ushirikiano walio uonesha kipindi chote cha mafunzo, ziara za vituoni na uandaaji wa rasimu ya ripoti ya mrejesho kwa wataalam wa idara ya afya na wadau wote kwa ujumla. Maarifa tuliyoyapata ni hazina kwa wilaya yetu hivyo natoa rai kwa kila mmoja ayatumie kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa na timu na hatimaye kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ndani ya wilaya yetu ya Magu.

Asanteni Sana

Ndg. Redemtus Deus

**Mwenyekiti, Timu ya SAM Magu**

**(Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi - Kituo cha Afya Kisesa)**

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AKDN** | Aga Khan Development Network |
| **CHMT** | Council Health Management Team (Timu ya Menejimenti ya Afya ya Halmashauri) |
| **CHF** | Community Health Fund (Mfuko wa Afya wa Jamii) |
| **CMT** | Council Management Team (Timu ya Menejimenti ya Halmashauri) |
| **CSO** | Civil Society Organization (Asasi za Kiraia) |
| **DHSB** | District Health Service Board (Bodi ya Afya ya Wilaya) |
| **HFGC** | Health Facility Govening Committee (Kamati ya Usimamizi wa Kituo) |
| **IMPACT** | Improving Access to Maternal and Newborn Health in Mwanza (Mradi wa Kuboresha Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto mkoa wa Mwanza) |
| **RCH** | Reproductive and Child Health (Afya ya Uzazi na Watoto) |
| **SAM** | Social Accountability Monitoring (Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii) |
| **WDC** | Ward Development Committee (Kamati ya Maendeleo ya Kata) |
| **WEO** | Ward Executive Officer (Afisa Mtendaji wa Kata) |

# Kutoka kwa Mkurugenzi

Ripoti hii ni sehemu ya matokeo ya utekelezaji wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (SAM) unaoendelea katika wilaya mbalimbali nchini.

Ripoti hii imeandaliwa kwa kushirikisha wananchi wa wilaya ya Magu baada ya kufanya ufuatiliaji shirikishi katika mifumo ya utoaji huduma za afya wilayani. Ufuatiliaji huu ulilenga katika kutathimini mchakato wa mipango katika maeneo ya mgawanyo wa rasilimali za afya, matumizi ya rasilimali hizo na utendaji wa vyombo vya usimamizi wa utoaji huduma za afya hususani zile zinazolenga afya ya uzazi, mama, baba na mtoto.

Utekelezaji ulifanyika kwa kutumia mbinu shirikishi ambapo wadau mbalimbali kwa kuzingatia uwakilishi wao walipatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo yaliyowawezesha kufanya uchambuzi wa taarifa za idara ya afya na hatimaye kufanya tathimini kwa kutumia dodoso kama lilivyoambatanishwa katika ripoti hii.

Matokeo yaliyopatikana yamechangia kuimarisha ushiriki wa pamoja wa watoa huduma, wananchi na wadau katika kuboresha huduma za afya hususani afya ya uzazi, mama baba na mtoto katika wilaya ya Magu kupitia majadiliano baina ya wananchi, wadau na timu ya menejimenti ya afya wilaya ya Magu na kuweka msingi wa awali wa maeneo muhimu ya kuboresha.

Vilevile, matokeo ya zoezi hili ni muhimu kwa wadau wa afya kwa kuwa yanatoa taarifa zinazo ainisha maeneo yanayohitaji kuboreshwa katika ujumla wake na pia yanaweza kutumika kama maelezo ya msingi (baseline information) katika kupima hali ya huduma ya afya ya msingi na maeneo muhimu ya kuboresha katika wilaya ya Magu.

Asanteni

**Irenei Kiria**

**Mkurugenzi Mtendaji**

# Yaliyomo

**Shukrani** 2
**Orodha ya Vifupisho** 3
**Kutoka kwa Mkurugenzi** 4
**Yaliyomo** 5
**Muhtasari** 6

**SEHEMU YA KWANZA** 7
1.0 Utangulizi 7
1.1 Dhana ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii 7
1.2 Malengo ya SAM 7
1.3 Mbinu za Utekelezaji wa SAM 7

**SEHEMU YA PILI** 9
2.0 Matokeo ya Uchambuzi wa Nyaraka na ziara Vituoni 9
2.1 Tathimini ya Uandaaji wa Mipango naUtekelezaji wa Shughuli za Afya 9
2.1.1 Utawala na Fedha 10
2.1.2 Dawa, vifaa na vifaa tiba 11
2.1.3 Afya ya uzazi, mama, baba na mtoto 13
2.1.4 Rasilimali watu katika sekta ya afya 14
2.1.5 Miundombinu na Mifumo ya Maji na Umeme 16
2.2 Tathimini ya Ufanisi wa Sheria, Miongozo na Taratibu za Utoaji Huduma za Afya 19
2.2.1 Ufanisi wa sheria, miongozo na taratibu za kazi 19
2.2.2 Kuzuia na kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za afya 19
2.2.3 Tathimini ya Utendaji wa Vyombo vya Usimamizi wa Uwajibikaji 20

**SEHEMU YA TATU** 23
3.0 Hitimisho 23
3.1 Mapendekezo 23
3.2 Mpango kazi wa pamoja 23

**Viambatanisho** 25

# Muhtasari

Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii ama Social Accountability Monitoring (SAM) ni dhana inayotekelezwa na jamii ili kuchangia uimarishaji wa mifumo ya utoaji wa huduma bora ya afya kwa kushirikisha wananchi katika kupanga, kusimamia na kufuatilia uwajibikaji wa watoa huduma katika ngazi zote ndani ya maeneo yao. Utekelezaji wa dhana hii pia unakumbusha wajibu kwa wenye dhamana ya kutoa huduma kwa kuzingatia kanuni na miongozo iliyopo ili kufikia haki za msingi za watumia huduma.

Utekelezaji wa zoezi la SAM Wilayani Magu uliwezesha wananchi kujengewa uwezo kuhusu Ufuatiliaji na Uwajibikaji. Hii iliwezesha kufanya uchambuzi wa nyaraka, uhakiki vituoni na tathmini ya hali ya utoaji wa huduma za afya. Hivyo, baadhi ya mambo yaliyobainika ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya ya uzazi, baba, mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma, uwepo wa dawa na vifaa tiba kwa hali ya kuridhisha, pamoja na uwepo wa mashimo ya kutupia kondo la nyuma na vichomea taka kwa vituo vyote vilivyotembelewa. Hali hii inachangia kuboresha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Pamoja na mafanikio yaliyoonekana pia idara ya afya Magu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa watumishi wa kada zote; baadhi ya watumishi kutozingatia maadili ya kazi; mkanganyiko katika uandishi wa nyaraka mbalimbali za vituo; baadhi ya vituo kuwa na mipango miwili tofauti kwa mwaka mmoja; uchangiaji hafifu mfuko wa CHF; mwingiliano wa wanasiasa kwenye shughuli za utendaji za vituo; vituo kukosa takwimu za makundi mbalimbali yanayohudumiwa; uhaba wa majengo kwa ajili ya huduma za uzazi, baba, mama na mtoto; pia vituo kukosa maji safi na salama.

Aidha, uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu (CMT na CHMT) umeahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa vituo pamoja wananchi wa maeneo husika kutatua changamoto mbalimbali zilizoibuliwa na timu. Pia uongozi umeahidi kutoa ushirikiano kwa timu ya SAM pindi watakapofanya ziara vituoni kutathmini mabadiliko.

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Huduma ya afya ya uzazi, mama na mtoto ni miongoni mwa vipaumbele vya mwanzo vya Wizara ya Afya. Serikali kwa kuzingatia umuhimu mkubwa imejidhatiti kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa kupitia mbinu tofauti tofauti ikiwemo ushirikishwaji wa jamii kupitia mfumo wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii kama ilivyobainishwa katika mpango mkakati wa nne (HSSP IV) wa afya. Hivyo, katika jitihada za kushiriki kuboresha huduma hii, Sikika kwa kushirikiana na Agha Khan Foundation waliamua kutekeleza mradi wa kuimarisha ushiriki wa jamii na uwajibikaji kupitia mfumo wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii, wilayani Magu.

## 1.1 Dhana ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii

Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii yaani Social Accountability Monitoring (SAM) ni dhana shirikishi kati ya wananchi (wenye wajibu na haki) na watendaji (wenye wajibu na dhamana), kwa pamoja kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu ya jamii bila ya ubaguzi kwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo nchini kwa kuzingatia kanuni na miongozo.

## 1.2 Malengo ya SAM

Lengo kuu la zoezi la SAM wilayani Magu ni kuimarisha mifumo ya usimamizi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya ikilenga afya ya uzazi kwa mama na mtoto kwa kuzingatia.

**Malengo Mahsusi;**

i. Kutathmini mchakato wa mipango na mgawanyo wa rasilimali afya hususani katika bidhaa za dawa na vifaa tiba, rasilimali watu na usimamizi wa fedha za afya ya uzazi, baba, mama na mtoto.
ii. Kulinganisha mgawanyo wa bajeti na matumizi ya dawa, rasilimali watu na afya ya uzazi, baba, mama na mtoto katika mpango kabambe wa afya
iii. Kutathmini usimamizi wa rasilimali watu, bidhaa za afya, miundombinu na utoaji huduma za afya ya uzazi, baba, mama na mtoto kwa mujibu wa mpango kabambe wa afya
iv. Kutathmini usimamizi wa uadilifu kwa umma na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za afya ya uzazi, baba, mama na mtoto.

## 1.3 Mbinu za Utekelezaji wa SAM

Utekelezaji wa zoezi la SAM ulihusisha taratibu za kutambulisha mradi wa IMPACT na kukutanisha wadau mbalimbali na watoa huduma za afya ili kupata timu ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii ya wilaya. Wilayani Magu, mchakato wa SAM uligawanyika katika hatua mbalimbali yaani; Utambulisho kwa viongozi wa halmashauri ili kupata idhini ya utekelezaji wa zoezi na timu

kupewa nyaraka muhimu za mafunzo na uchambuzi, pia kufanya mikutano ya jamii ili kupata ushiriki wa wananchi. Jumla ya wananchi wanne (4) mmoja kwa kila kata walichaguliwa kidemokrasia kupitia mikutano ya jamii katika kata za Isandula, Kisesa, Nyangunge na Kabila.

Kwa upande wa Baraza la Madiwani, walichaguliwa wawakilishi 2 (KE na ME) kupitia Kamati ya Huduma za Jamii. Kwa kutambua umuhimu na mchango wa wadau katika kuhimiza Utawala Bora na kuimarisha mifumo ya utoaji na usimamizi wa huduma bora za afya hususan za mama, baba na mtoto, Sikika pamoja na Aga Khan Foundation walikutana na wadau kwa madhumuni ya kutambulisha mradi wa IMPACT, dhana ya SAM na utekelezaji wake. Baada ya utambulisho na majadiliano katika mkutano wa wadau wa afya, makundi ya uwakilishi yalitumia demokrasia kuchagua mwakilishi mmoja kwa kila kundi ambao kwa pamoja waliunda timu ya SAM ya Wilaya yenye jumla ya wajumbe 15 na kutambulishwa rasmi kwa wadau wote.



**Fredrick Ngao kutoka Sikika akielezea juu ya dhana ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (SAM) kwa wananchi wa kata ya Isandula, wilayani Magu.**

# SEHEMU YA PILI

Katika sehemu hii timu inabainisha matokeo yaliyopatikana baada ya uchambuzi wa nyaraka za halmashauri, za vituo na uhakiki uliofanywa katika vituo 15 vya kutolea huduma katika wilaya ya Magu. Pia inaeleza kuhusu mjadala uliofanyika kati ya timu ya SAM, uongozi wa halmashauri (CMT na CHMT) pamoja na makubaliano ya namna watakavyoshughulikia changamoto mbalimbali zilizoibuliwa na timu ya SAM.

## 2.0 Matokeo ya Uchambuzi wa Nyaraka na ziara Vituoni

Katika uchambuzi wa nyaraka za idara ya afya na ziara ya uhakiki vituoni kwa vituo 15 vya mradi wa IMPACT, timu ya SAM ilibaini maswala mbalimbali yaliyosaidia kuandaa taarifa kutoka katika maeneo ya uandaaji wa mipango na utekelezaji. Uchambuzi huo ulilenga maeneo ya: - utawala na fedha, afya ya uzazi, baba, mama na mtoto, bidhaa za afya, rasilimali watu, miundo mbinu ya afya, na ushiriki wa wadau na jamii.

## 2.1 Tathimini ya Uandaaji wa Mipango na Utekelezaji wa Shughuli za Afya

Timu ilipata nyaraka za mipango na ripoti za idara ya afya ambazo ziliiwezesha kufanya uchambuzi na tathimini ya kina kuhusu hali ya utoaji wa huduma za afya wilayani.





**Mjumbe wa timu ya SAM, Bw. Samson Mathayo akiwasilisha kazi ya kikundi wakati wa uchambuzi wa taarifa za idara ya Afya.**

### 2.1.1 Utawala na Fedha

*Uandaaji wa Mipango kwa Kuzingatia miongozo*


Ukiachia mbali vituo kuwa na mipango, kamati za kuandaa mipango kuwepo na mipango yote katika vituo 15 kuidhinishwa kwa asilimia 100, changamoto ilionekana katika utoaji wa mafunzo ya kuandaa mpango na uwepo wa miongozo ya kuandaa mipango vituoni. Katika vituo 15 vilivyotembelewa, vituo 14 (93%) vilikuwa na mipango kazi ya mwaka huku vituo 11 (73%) kamati zake zilipatiwa mafunzo ya namna ya kuandaa mipango. Changamoto nyingine zilihusisha; kuandaa mpango kwa kutofuata muongozo, baadhi ya vituo kunakili mipango na taarifa za mipango ya vituo vingine (copy and paste) mfano; mipango ya kituo cha Afya Kabila na Kahangara inafanana, pia Kisesa na zahanati ya Bujashi muhtsari wa utekelezaji inafanana.




**Kielelezo Na. 1: Tathimini ya maandalizi ya mipango ya afya katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**


*Mgawanyo wa bajeti ya afya kutoka vyanzo mbalimbali*

Kiasi kikubwa cha fedha kimeonekana kuelekezwa katika chanzo cha vyanzo vingine (47%) kikifuatiwa na mfuko wa dunia (14%) pamoja na mfuko mkuu wa pamoja wa serikali za mitaa (13%). Vyanzo vingine vimeonekana kuwa na kiasi kidogo. Hata hivyo, chanzo cha papo kwa papo ambacho kimeonesha kuwa na asilimia sifuri (0) tofauti na uhalisia kuwa vyanzo mbadala vya CHF na NHIF havijaweza kuwa na asilimia 100.




**Kielelezo Na. 2: Tathimini ya mgawanyo wa bajeti ya afya kutoka katika vyanzo tofauti tofauti. Chanzo; Ripoti ya utekelezaji wa CCHP – Magu, 2017/18.**

*Makisio ya bajeti na matumizi ya fedha za idara ya afya*
Mwaka 2017/18, idara ya afya ilitenga jumla ya shilingi 5,919,641,566/= kwa matumizi ya shughuli malimbali bila ya kuhusisha shilingi 115,315,028/= zilivuka mwaka toka 2016/17. Shilingi 2,256,295,418/= sawa na asilimia 38 zilipokelewa na kutumia shilingi 2,072,327,890/= sawa na silimia 35.




**Kielelezo Na. 3: Tathimini ya makisio ya bajeti na matumizi ya fedha za afya. Chanzo; Ripoti ya ytekelezaji wa CCHP – Magu, 2017/18.**


### 2.1.2 Vifaa vya afya, dawa, na vifaa tiba

*Bajeti ya vifaa vya afya, dawa na vifaa tiba*
Uchambuzi wa bajeti ya dawa na vifaa tiba katika ripoti za utekelezaji kwa chanzo cha MSD mwaka 2017/18 ulionesha mpango wa bajeti ya dawa na vifaa tiba ulikuwa na kiasi cha shilingi 664,264,611.29 na kupokelewa kiasi cha 448,661,865.28 pia mwaka 2018/19 ziliombwa shilingi 729,152,240.38 na kupokelewa 413,939,950.00, hata hivyo vyanzo vingine vya fedha kama Mfuko wa pamoja, NHIF/CHF na RBF vimeonesha tu kiasi cha fedha zilizoombwa ila timu haikuweza kupata kiasi kilichopokelewa.

*Upatikanaji wa dawa*
Uchambuzi umeonesha kuwa vituo vyote 15 vilivyotembelewa vilibainisha mahitaji yake ya dawa na vifaa tiba katika mipango na bajeti. Kwa mwaka 2017/18, vituo vilitoa taarifa ya uwepo wa dawa muhimu kwa wastani kati ya asilimia 95 - 100. Aidha, kwa mwaka 2018/19 upatikanaji umeonekana kwa wastani wa asilimia 75 hadi 90. Vituo vimeripoti upungufu wa baadhi ya vifaa na dawa kama *paracetamol, Septrine, folic acid, metronidazole na gloves.* Hata hivyo, hali ni tofauti katika hospitali ya wilaya kwani kwa mwaka 2017/18 hali ya dawa muhimu ilikuwa ni asilimia 70 huku mwaka 2018/19 upatikanaji ukiwa asilimia 100. Hata hivyo timu imebaini kuwa baadhi ya mahitaji hayana uhalisia. Mfano; mpango kazi wa hospitali ya wilaya ya Magu ulionesha kuwa na hitaji la mashine za mionzi (X-ray 15) ambapo si uhalisia wa mahitaji ngazi ya hospitali ya wilaya.

*Utunzaji wa dawa na vifaa tiba*


Vituo 14 kati ya 15 viliripoti uwepo wa kabati za kutunzia dawa isipokuwa zahanati ya Chanduru. Hata hivyo, idadi kubwa ya vituo vina kabati chache kati ya (1-2) na baadhi ni ndogo sana. Mfano; zahanati ya Ijinga kabati na shelfu haziridhishi kabisa kuhifadhi dawa na vifaa kutokana na udogo na kutengenezwa chini ya kiwango. Katika zahanati ya Chanduru hapakuepo na kabati kabisa na dawa zote huhifadhiwa kwenye shelfu dogo. Kwa upande wa utunzaji kumbukumbu, vituo vyote 15 hutunza kumbukumbu za uagizaji na upokeaji wa dawa kwenye leja na pia baadhi ya taarifa zipo kwenye mbao za matangazo kwa ajili ya matumizi ya umma. Hata hivyo, pamoja na changamoto za miundombinu ya kutunzia dawa zilizobainika, uongozi wa vituo vya huduma na CHMT ulibainisha mipango endelevu ya kutatua baadhi ya changamoto kwa kuziweka kwenye bajeti ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba.




**Kielelezo Na. 4: Tathimini ya hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Hali ya upatikanaji wa vifaa vya afya na vifaa tiba*


Katika vituo vyote 15, mashine za kupimia BP na vitanda vilikuwepo kwa asilimia 100. Suala la kuvutia ni kuwa katika vituo vyote vifaa vilivyopo vimeonekana vyote kufanya kazi. Aidha, ukosefu wa vifa vingine umesababisha huduma muhimu zikiwemo za vipimo vya ultra sound hazipatikani katika vituo vya afya kama, Kabila, Kisesa, Nyanguge, na Kahangara. Kituo cha afya Lugeye mashine zipo lakini hazifanyi kazi kutokana na kutokuwepo wataalam. Ukosefu wa baadhi ya huduma vituoni huathiri utolewaji wa huduma kwa akina mama wajawazito na kusababisha ongezeko la rufaa na mlundikano wa wagonjwa katika hospitali ya wilaya.




**Kielelezo Na. 5: Tathimini ya hali ya upatikanaji wa vifaa vya afya na vifaa tiba katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Mfumo wa mnyororo baridi*

Vituo vyote 15 vifadhi dawa za chanjo kwenye mfumo wa mnyororo baridi kwa kutumia deli au jokofu. Mfumo huo hutumia ama umeme wa TANESCO au umeme wa Sola japo kwa upande wa jokofu ama deli, baadhi ya vituo vina vifaa vyote viwili wakati vingine vikiwa na kimojawapo kulingana na mahitaji ya kituo. Vituo 13 (87%) vilikuwa na jokofu huku vituo 14(93%) vilikuwa na deli. Kwa upande wa nishati itumikayo kuendesha vifaa hivyo, vituo 10 (67%) hutumia umeme wa TANESCO na vituo 5 (33%) hutumia umeme wa Jua.




**Kielelezo Na. 6: Tathimini ya hali ya mfumo wa mnyororo baridi katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

### 2.1.3 Afya ya uzazi, mama, baba na mtoto

Huduma za afya ya uzazi, mama, baba na mtoto hutolewa bure kwenye kila kituo cha huduma kwa kufuata miongozo na sera za wizara ya afya. Wilaya ya Magu imeendelea kuboresha huduma hizi kwenye vituo vyake kadiri fedha zinavyopatikana. Hospitali ya wilaya inafanya ukarabati wa majengo ya kitengo cha mama na mtoto na vituo vya afya 4 vimefanya upanuzi wa majengo ili kuboresha huduma hizi. Hata hivyo, timu ya SAM ilibaini baadhi ya changamoto kwenye vituo kwa huduma za mama, baba na mtoto.

*Hali ya afya ya uzazi, mama, baba na mtoto*


Vituo vyote 15 vimeeleza kuwa hakuna vifo vya uzazi kwa mgawanyiko wa wajawazito na watoto wakati wa kujifungua ndani ya saa 24, chini ya mwaka mmoja kwa kila kituo (ndani na nje ya kituo) kwa mwaka 2017/18 na mwaka 2018/19. Hata hivyo, kwa mujibu wa CCHP - ngazi ya hospitali ya wilaya, hakuna vifo vya watoto chini ya miaka 5 vilivyotokea ndani ya saa 24 hadi wiki 6 lakini katika CCHP hiyo hiyo - uk. 23 jedwali Na. 9, vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimeonekana kuwa 84 na kuelezea sababu ya vifo hivyo. Vile vile (CCHP - jedwali Na. 11) limeonesha idadi ya vifo vya akina mama wakati wa ujauzito na kujifungua vikiwa 10 ndani ya kituo na 7 kwenye jamii.

Hata hivyo ufafanuzi wa idara ya afya ulibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa maana ya takwimu za 2017, Hospital ya wilaya ilikuwa na vifo vya uzazi 11 (Hospitali - 10 na kwenye jamii ni 1), kituo cha Kisesa "A" vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 2 (kituoni - 1 na 1 - kwenye jamii), Zahanati ya Mwamabanza kulikuwa na kifo 1 kwenye jamii kitokanacho na uzazi na Lugeye kulikuwa na kifo 1 cha kwenye jamii.

*Hali ya huduma ya afya ya uzazi, mama, baba na mtoto vituoni*
Hospitali ya wilaya inaudumia watoto chini ya miaka mitano kati ya 120 hadi 250. Aidha, Vituo vya afya vinahudumia watoto chini ya miaka 5 kati ya 60 hadi 150 huku zahanati zikihudumia kwa wastani wa 30 hadi 50 kwa siku. Zahanati ya Ijinga ndiyo inayohudumia watoto wachache kwa wastani wa watoto 2 hadi 3 kwa siku. Aidha, vituo vyote 15 vilibainisha uwepo wa watoa huduma wawili ndani ya jamii ambao hutoa elimu ya kubaini vihatarishi wakati wa ujauzito na kuwahi kituoni wakati wa kujifungua na kupata chanjo. Mfano, zahanati ya Mwamanga, awali akina mama waliokuwa wanajifungulia kituoni walikuwa 7-10 kwa mwezi ila kwa sasa wameongezeka hadi kufikia 30 kwa mwezi. Kituo cha afya Nyanguge akina mama wanaopata huduma na kujifungulia kituoni wameongezeka kutoka 28-30 kwa mwaka mpaka 70-80.

*Huduma za rufaa*
Vituo vyote vilivyotembelewa na timu vinatoa huduma za rufaa kwa wagonjwa wa dharura hususani wajawazito walioshindwa kujifungua katika kituo husika. Pia katika vituo vilivyotembelewa, kuna magari ya wagonjwa matano (5), yakiwa ni Hospitali ya wilaya (1), kituo cha afya Kisesa (1), Kabila (2) na Lugeye (1) magari yote yapo katika hospitali ya wilaya na huwafuata wagonjwa pindi rufaa inapohitajika, hii inatokana na changamoto ya jiografia ya wilaya na ukosefu wa madereva. Hata hivyo, timu ilibaini kuwa wajawazito wanachangia gharama za usafiri wa gari. Mfano; kituo cha afya Kabila na Lugeye, wajawazito hulipia shilingi 21,000/=.


### 2.1.4 Rasilimali watu katika sekta ya afya
*Hali ya upatikanaji wa watumishi wa afya*
Timu ilifanikiwa kufanya uchambuzi wa mahitaji ya rasilimali watu kwa ngazi zote za vituo na kutembelea vituoni. Uchambuzi ulibaini kuwa mwaka 2017/18 idara ya afya ilikuwa na watumishi 545 kati ya 720 sawa na asilimia 76 waliokuwa wanahitajika na kwa mwaka 2018/19 idara ina watumishi 585 kati ya 720 sawa na asilimia 81 wanaohitajika kwa ajili ya kutoa huduma ngazi mbalimbali.




**Kielelezo Na. 7: Tathimini ya hali ya upatikanaji wa watumishi wa afya wilayani Magu. Chanzo; CCHP – Magu, 2017/18.**

*Hali ya utoaji wa stahiki za watumishi wa afya*


Vituo 14 (93%) kati ya vituo 15 (100%) vilivyotembelewa vilithibitisha watumishi wake kupatiwa malipo ya sare za kazi (vitambaa). Ukiondoa hospitali ya wilaya ambayo ndio pekee watumishi wake hustahili kulipwa malipo ya muda wa dharura, malipo ya muda wa ziada yalionekana kutolewa kwa kiasi kidogo kwani ni vituo 2 (13%) ambavyo vilithibitisha watumishi wake kulipwa stahiki hiyo.




**Kielelezo Na. 8: Tathimini ya hali ya malipo ya stahiki mbalimbali za watumishi wa afya katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Mafunzo kazini kwa watumishi wa afya*

Vituo vyote 15 vilivyotembelewa ilithibitika kutolewa mafunzo ya kujengewa uwezo kwa watumishi. Hata hivyo, utoaji wa mafunzo ya TB (67%) umeonekana kuwa wa kiwango cha chini ukilinganisha na mafunzo mengine kama MTUHA (100%), CTC/PMTCT (93%), huduma za mama, baba na mtoto (93%) ambayo utoaji wake umekuwa wa kiwango cha juu.




**Kielelezo Na. 9: Tathimini ya hali ya utoaji mafunzo kazini kwa watumishi wa afya katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Usimamizi shirikishi*

Pamoja na uhalisia kuwa, vituo vyote 15 sawa na asilimia 100 vilithibitisha kufanyiwa usimamizi shirikishi, vituo 14 sawa na asilimia 93, watoa huduma wake walieleza kuwa usimamizi shirikishi na kujiwekea mipango ya kutatua changamoto kwa pamoja vina mchango mkubwa katika kuboresha huduma zitolewazo. Tathimini ya utendaji kazi kwa kuzingatia mfumo wa (OPRAS) ilibainika kufanyika vituoni japo baadhi ya watoa huduma walieleza changamoto ya kutokuwa na uelewa wa kina juu ya malengo ya utendaji kama yalivyoainishwa katika fomu za OPRAS. Mfano; zahanati ya Mahaha, Chanduru na Ijinga mara ya mwisho kujaza fomu ilikuwa katika kipindi cha mwaka 2016/17.


### 2.1.5 Miundombinu na Mifumo ya Maji na Umeme

*Majengo ya vituo vya kutolea huduma*

- Katika ziara ya uhakiki vituoni timu ilibaini kuwa vituo 9 kati ya 15 vilivyotembelewa havina majengo maalumu ya RCH isipokuwa hospitali ya wilaya Magu, Kituo cha afya Kahangara, Kisesa, zahanati za Ihayabuyaga, Bujashi na Buhumbi.
- Pia, baadhi ya vituo kama zahati ya Ijinga hutoa huduma za mama na mtoto (RCH) kwenye veranda ama kutengewa chumba/eneo dogo la jengo hali inayosababisha kutokuepo kwa usiri.
- Baadhi ya vituo vya huduma vina majengo chakavu na ufinyu wa maeneo ya huduma za mama na mtoto (RCH). Mfano; zahanati za Ijinga, Busaranga, Chanduru, Mwamanga, Bujashi, kituo cha afya Kisesa na hospitali ya wilaya.
- Timu ilibaini vituo 13 kati ya 15 vilivyotembelewa vina nyumba za watumishi na vituo 2 havina nyumba. Baadhi ya nyumba za watumishi hazina vyoo hali inayofanya watumishi na familia zao kutumia vyoo vilivyopo kituoni. Mfano; Bujashi, Mwamanga, Lutale na Chandulu.

*Nyumba za watumishi wa afya*


Vituo 13 kati ya 15 vilikuwa na nyumba za watumishi zilizo katika hali tofauti tofauti za ubora. Vituo 2 (13%) kati ya 15 vilikuwa na nyumba za watumishi zenye hali nzuri, vituo 7 (47%) nyumba zake zilikuwa na ubora wa wastani huku vituo 4 (27%) nyumba zake ziko katika hali isiyoridhisha. Baadhi ya nyumba za watumishi ambazo ni chakavu zipo katika kituo cha afya Lugeye, zahanati ya Busalanga na Ijinga.




**Kielelezo Na. 10: Tathimini ya hali ya ubora wa nyumba za watumishi wa afya katika vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Hali ya vyoo na usafi wa mazingira*

Vyoo katika vituo 6 (40%) kati ya vituo 15 vilikuwa na hali nzuri. Vituo 8 (53%) vyoo vyake vilikuwa na hali ya wastani huku kituo 1 (7%) kikiwa na hali ya vyoo isiyoridhisha. Kwa upande wa tathimini ya mazingira ya vyoo kwa watu wenye ulemavu, vituo 3 (20%) ndivyo vilikuwa na vyoo angalau vinavyokidhi mazingira ya watu wenye ulemavu. Mfano; Kituo cha afya Nyanguge pekee ndicho chenye choo kilichokidhi kwa asilimia 100 mahitaji ya watu wenye ulemavu. Vituo vya Nyanguge, Kabila, Ijinga na Mwamabanza havikuwa na mazingira safi na salama.





**Kielelezo Na. 11: Tathimini ya hali ya vyoo na usafi wa mazingira ya vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Hali ya vizimba vya kuchomea taka na shimo la kutupia kondo la nyuma la uzazi*
Takribani vituo 14 (93%) kati ya vituo 15 vina vizimba vya kuchomea taka na shimo la kutupia kondo la nyuma ambavyo vimezungushiwa uzio ingawa havifungwi na kufuli. Uongozi umeahidi kununulia kufuli maeneo yote timu iliyobaini.


Hata hivyo, baadhi ya vituo mfano; zahanati ya Chanduru wanatumia shimo la kawaida kutupa taka hatarishi, na kizimba cha kituo cha afya Kisesa ni kidogo na kipo katika hali mbaya (kimebomoka) kinahitaji kujengwa upya.

Katika kituo cha afya Nyanguge, kuna shimo la kutupia kondo la nyuma lakini halitumiki. Pia, Wananchi katika zahanati ya Busalanga wamelalamika kuwa makondo ya nyuma hutupwa katika mto hivyo kuchangia uharibifu wa mazingira japo CHMT waliahidi kufuatilia na kupata ufumbuzi.




**Kielelezo Na. 12: Tathimini ya hali ya vichomea taka na mashimo ya kutupia kondo la nyuma la uzazi katika vituo 15 vya kutolea huduma. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Mfumo wa maji safi na umeme*
Vituo vilivyotembelewa na timu vimeonesha kuwa asilimia 27 (4) tu vina mfumo wa maji ya bomba, asilimia 53 (8) vinategemea maji ya mvua ilihali asilimia 20 (3) vinategemea maji ya visima. Hali hii inadhihirisha hakuna mfumo wa maji safi na salama ya kutosheleza mahitaji ya vituo hasa nyakati za kiangazi.




**Kielelezo Na. 13: Tathimini ya upatikanaji wa maji safi na salama katika vituo 15. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Ulinzi wa kituo na usalama wa watumishi*

Vituo vyote 15 vilivyotembelewa (isipokuwa hospitali ya Wilaya), havina uzio kuzunguka eneo la kituo. Hali hii huhatarisha sio tu usalama wa watumishi bali hata rasilimali za kituo. Mfano, katika kituo cha afya Kabila na Kahangara, watumishi wanalalamika wananchi kuingia ovyo ndani ya eneo la kituo muda wa kuhudumia wagonjwa na sio muda wa kutembelea wagonjwa kama inavyoelekezwa. Katika zahanati ya Busalanga, watumishi wameripoti kutishiwa usalama wao kwani wananchi wanaingilia eneo la kituo na kufanya shughuli za kijamii zikiwemo kukata miti, kulima, kuingiza mifugo. Vile vile, vituo vyote vimeripoti kuwa na walinzi ambao wanalipwa na kijiji, isipokuwa vituo vya Kisesa, Kabila na Bujashi. Hata hivyo vituo hivyo vina mlinzi mmoja mmoja ambao pia hawalipwi kwa wakati hali inayoathiri utendaji kazi wao na baadhi ni wazee sana.

## 2.2 Tathimini ya Ufanisi wa Sheria, Miongozo na Taratibu za Utoaji Huduma za Afya

Utoaji wa huduma ya afya nchini huongozwa na sheria pamoja na taratibu. Uchambuzi na uhakiki wa timu ulitathimini namna idara ya afya na jamii wanavyotekeleza wajibu na majukumu mbalimbali kwa kuzingatia sheria na taratibu.

### 2.2.1 Ufanisi wa sheria, miongozo na taratibu za kazi


Timu ilifanya tathmini ya Ufanisi wa Sheria, Miongozo na Taratibu za Utoaji Huduma za Afya kwani utoaji wa huduma za afya huongozwa na sheria, miongozo na taratibu mbalimbali, hata hivyo timu ilifanikiwa kubaini yafuatayo.

- Vituo vyote vina nakala za miongozo inayotumiwa na sekta ya afya japo kuwa kuna changamoto katika matumizi yake hasusani uandaaji wa mipango, taarifa, ufanyaji kazi wa kamati za vituo n.k,
- Pia bado kuna watumishi hawavai sare na vitambulisho wawapo kazini kinyume na taratibu.
- Bado kuna ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa afya hususani kutumia lugha mbaya, kupigana na wagonjwa na kuwadhalilisha akina mama waendapo kliniki. Mfano; katika kituo cha afya Kabila wananchi wamemlalamikia mtoa huduma wa kitengo cha RCH kwa kutumia lugha ya matusi na mara nyingine kufikia kupigana na wagonjwa ila mara zote wagonjwa ndio wanachukuliwa hatua za kisheria kwa madai ya kumfanyia fujo muuguzi katika eneo la kazi.
- Pia ikitokea mama amepoteza kadi ya kliniki hulazimika kununua kadi hiyo kwa shilingi 1000/- kutoka katika duka la dawa lililopo kijijini hapo. Mfano; zahanati ya Mahaha na katika kituo cha afya Lugeye.

### 2.2.2 Kuzuia na kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za afya

Kwa mujibu wa CHMT, kamati za usimamizi wa vituo zimekuwa na mchango mkubwa katika uongozi wa vituo. Kamati na watumia huduma wamekuwa sehemu muhimu ya uangalizi wa mwenendo wa huduma na watoa huduma kwa ujumla.

*Mifumo ya kutoa maoni na kupokea malalamiko vituoni*
Vituo 13 (87%) kati 15 vilivyotembelewa vina masanduku ya maoni lakini hayatumiki ipasavyo. Vituo 11 (73%) wananchi hutumia kamati za afya na mikutano ya jamii kutoa maoni ama malalamiko.





**Kielelezo Na. 14: Tathimini ya mifumo ya kutoa maoni na malalamiko katika vituo 15. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2109.**

Pia njia nyingine za kutolea maoni zilizobainishwa na watoa huduma ni kupitia mikutano ya jamii kwa asilimia 73, viongozi wa kijiji asilimia 6 na simu za viongozi/madiwani asilimia 53. Njia nyingine ni pamoja na kumfuata mtumishi mwingine kituoni na kuandika kwenye daftari la kutolea maoni lililopo kituoni hapo mfano zahanati ya Kinango na Busalanga.

Watumishi wameripoti kuwa masanduku hufunguliwa kila baada ya robo mwaka na mara nyingine hufunguliwa kila mwezi. Hata hivyo, baada ya timu kuulizia ni maoni mangapi kituo kiliwahi kukusanya, vituo vingi walisema hawakuwahi kukuta karatasi yoyote ya maoni.

### 2.2.3 Tathimini ya Utendaji wa Vyombo vya Usimamizi wa Uwajibikaji

*Kamati za usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya*
Vituo 11 (73%) kati ya 15 vilivyotembelewa vina kamati ili hali vituo 4 havina. Kati ya vituo 11 (73%) vyenye kamati, wajumbe wake hawjapatiwa mafunzo elekezi ya wajibu na majukumu yao. Pia, timu ilibaini kuwa kamati zimepitiliza muda wake tangu ziundwe. Kamati zinakutana kila robo mwaka na katika baadhi ya vituo wajumbe wanalipwa posho na nauli za vikao. Mfano; Kahangara na Buhumbi wakati zahanati ya Mahaha wajumbe walilamika kutolipwa posho. Hata hivyo, katika hospitali ya Magu, watumishi waliripoti kuwa kamati ya kituo haihusiki katika kuhakiki dawa zinazopokelewa kituoni bali kamati inayohusika na uagizaji wa dawa (theraupetical committee) ndio wanaohusika. Aidha, timu ilibaini kuwa vituo 8 kati ya 15 vina nakala ya muongozo wa uendeshaji wa kamati. Pia, nakala zinapatikana kwa Mganga Mfawidhi na siyo kwa wajumbe hivyo hawaelewi namna bora ya uendeshaji wa kamati zao.




**Kielelezo Na. 15: Tathimini ya uwepo na hali ya utendaji kazi wa kamati za usimamizi wa vituo 15 vya kutolea huduma za afya. Chanzo; Uhakiki wa timu ya SAM, 2019.**

*Baraza la madiwani na bodi ya afya ya wilaya*

Kupitia nyaraka za mihutasari, timu ilibaini kuwa vyombo hivi muhimu vya usimamizi hukutana kwa kila robo mwaka na kupokea taarifa za utekelezaji, kuzijadili na kutolea maelekezo yanayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma. Hata hivyo, timu ilibaini kuwa vyombo hivi vimesaidia kuongezeka kwa vituo vya huduma kwa idadi toka 39 kwa 2016/17 hadi 43 kwa 2019 halmashauri ya Magu, pia miundombinu inaendelea kuboreshwa ili kuhudumia watu wengi zaidi na kwa ubora.

**Changamoto za jumla kwenye vituo vya huduma**

Timu ya SAM wilayani Magu ilibaini mambo mbalimbali kama changamoto katika uchambuzi wa taarifa za idara ya afya na ziara ya uhakiki vituoni na inapendekeza uongozi wa halmashauri na idara kuyafanyia kazi ili kuboresha huduma zitolewazo hususan za mama, baba na mtoto yakiwa ni;

- Katika vituo 15 vilivyotembelewa na timu ilibainika ukosefu wa vitendea kazi muhinu mfano; kompyuta (laptop) za kuingizia takwimu muhimu za kituo kielektroniki na ni vituo 5 vyenye komputa za ofisi vingine ni za watumishi binafsi.
- Uandaaji wa mipango na taarifa kwa idara na vituo vya huduma bado ni changamoto haswa kenye takwimu na mpangilio
- Kutokuwepo na miundombinu bora ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma shelfu na kabati na pallets za kutosha.
- Upungufu kwa takriban asilimia 50 ya rasilimali watu katika vituo 15 vya huduma vilivyotembelewa na timu hii ikitoa taswira kwa hali ya Wilaya ya Magu
- Vituo havina uzio hali inayohatarisha usalama wa watumishi kutoa huduma dharura inapojitokeza usiku na pia rasilimali za kituo

- Kutokuwepo kwa utaratibu thabiti wa kutolea maoni ya wananchi, hususani masanduku ya maoni kwani kati ya vituo 15 vilivyotembelewa 13 yapo ila hayatumiki na mengi hayana funguo 2 ili kudhibiti upokeaji wa malalamiko.
- Upungufu na uchakavu wa miundombinu ya vituo zikiwemo nyumba za watumishi na vyoo kwani ni asilimia 13 pekee ya nyumba zilibainika kuwa nzuri.
- Ukosefu wa sare za watumishi, kwani vituo vingi vimeripoti kuwa ni wauguzi pekee ndio hupatiwa vitambaa vya sare na wanajitegemea gharama za kushona.
- Ukosefu wa huduma ya uhakika ya maji safi na salama katika vituo na usafi usioridhisha wa mazingira ya huduma.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 Hitimisho

Kwa kuwa dhumuni la utekelezaji wa SAM ni kuimarisha mifumo ya kutolea huduma za afya, timu inaamini kuwa masuala yote yaliyobainika na kuafikiwa kuboreshwa yatafanyiwa kazi kwa wakati. Pia, timu inaomba kupewa ushirikano wa kutosha wakati watakapokuwa wanafanya ziara za kufuatilia utekelezaji wa maazimio, maoni ya mara kwa mara na uboreshaji wa huduma katika vituo.

## 3.1 Mapendekezo

- Idara ya afya kupitia CHMT kuboresha mfumo mzima wa uandaaji, uhakiki na upokeaji wa taarifa za vituo vya huduma
- Kuboreshwa hali ya huduma za mama, baba na mtoto vituoni na kuweka mipango ya huduma za RCH kuwa ni ya wenza zaidi kabla, wakati na baada ya kujifungua
- Halmashauri kuweka mikakati ya kuboresha miundombinu ya afya vituoni pamoja na uwepo wa dawa na vifaa tiba vya kutosha kutolea huduma
- Idara kuendelea kubainisha mahitaji ya watumishi na kuomba kulingana na taratibu na kuwagawanya kulingana na uhitaji wa vituo vya huduma
- Halmashauri kuitumia ripoti ya SAM inayotokana na vituo 15 vya mradi wa IMPACT kuwa chachu ya maboresho kwa vituo vingine wilayani Magu
- Halmashauri na idara ya afya kuweka mikakati endelevu ya kuwashirikisha wadau kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa ngazi zote na jamii kuwa sehemu ya uwajibika na maboresho

## 3.2 Mpango kazi wa pamoja

Maeneo makuu yafuatayo yaliafikiwa kufanyiwa maboresho na wadau kama ifuatavyo:-

| NA | MPANGO KAZI WA PAMOJA | MUHUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Kutokana na changamoto ya uandaaji wa mipango CHMT wataendelea kutoa mafunzo elekezi na endelevu kwenye vikao vya kila robo mwaka vya watumishi wa vituo ili kuhakikisha wanaboresha mipango yao. | CHMT |
| 2 | CHMT wataelekeze watumishi ngazi za vituo kutofautisha fedha zinazokusanywa za papo kwa papo na zile za mfuko wa iCHF ili kuboresha mapato | CHMT |
| 3 | Waheshimiwa madiwani watakumbushwa kujikita katika majukumu na mipaka yao ya kiutendaji ili yasiingiliane na majukumu ya watumishi | DED na Mwenyekiti wa Halmashauri |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Afisa Ustawi wa Jamii wilaya kupitia ofisi ya Mkurugenzi atasimamia watumishi wa afya kuboresha mahusiano ya utendaji kazi wa maafisa ustawi wa jamii/kamati za afya za kata/watendaji wa kata na vijiji ili kuhakikisha wanatambua makundi yote ya msamaha na kutumia takwimu sahihi katika kuandaa mipango na bajeti zao. | CMT/DMO |
| 5 | Ili kupunguza matukio ya uzembe yanayofanywa na wauguzi katika wodi ya wazazi, Mganga Mkuu wa Wilaya na CHMT watafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vituo vya huduma na kukusanya maoni ya wananchi ili waweze kufahamu hali halisi ya huduma na uzingatiwaji wa maadili ya watumishi. | CHMT/DMO |
| 6 | Suala la uhamasishaji wa iCHF litakuwa ni mkakati endelevu na kipaumbele cha Halmashauri kupitia ofisi ya DC, DED na DMO. | DC, DED, DMO na Mratibu wa CHF |
| 7 | CHMT na waganga wafawidhi watasimamia kwa karibu uwepo na matumizi sahihi ya sanduku na daftari la maoni vituoni, pia uwekaji wa taarifa za wazi kwenye mbao za matangazo kwa kila kituo cha kutolea huduma. | CHMT, Waganga wafawidhi na HFGC |

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho Na.1**
**Vituo vilivyotembelewa**

1. Hospitali ya Wilaya ya Magu
2. Kituo cha afya Kisesa
3. Kituo cha afya Kabila
4. Kituo cha afya Lugeye
5. Kituo cha afya Nyanguge
6. Zahanati ya Ijinga
7. Zahanati ya Mwamabanza
8. Zahanati ya Lutale
9. Zahanati ya Kahangara
10. Zahanati ya Mahaha
11. Zahanati ya Bujashi
12. Zahanati ya Busalanga
13. Zahanati ya Kinango
14. Zahanati ya Mwamanga15
15. Zahanati ya Chanduru

**Kiambatanisho Na. 2**
Timu ya SAM wilaya ya Magu

| NA. | JINA | KUNDI LA UWAKILISHI | JINSI |
|---|---|---|---|
| 1. | AnethNzali | Wananchi | KE |
| 2. | Angelina Clementi | Kamati za Usimamizi wa Vituo | KE |
| 3. | ChachaGisuka | Asasi za Kiraia | ME |
| 4. | Lilian Alfred | CHMT | KE |
| 5. | MabulaPhilipo | Wananchi | ME |
| 6. | Marco Joseph M | Wananchi | ME |
| 7. | Marco M. Minzi | Madiwani | ME |
| 8. | Meckitrida Pius | Wananchi | KE |
| 9. | Philipo J. Lusesa | Mtendaji wa kata | ME |
| 10. | PraxedaMaketere | Vikundiakina mama | KE |
| 11. | Salome M. Nyalili | Bodi ya Afya ya Halmashauri | KE |
| 12. | Samson M. Mathayo | Vijana | ME |
| 13. | Sylivester M. Kakinda | Walemavu | ME |
| 14. | Velina E. Makwandi | Madiwani | KE |

## Kiambatanisho Na. 3

### A. Tathimini ya Mifumo ya Utoaji Huduma za Afya Ngazi ya Wilaya kwa Vituo Vilivyopo katika Mradi wa IMPACT

1. Tathimini ya Usimamizi wa Mipango

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Mpango wa mwaka uliopita CCHP ulifuata mwongozo wa CCHP toleo Na. 4? (4th ed.)? | |
| 2 | Bajeti kuu ya Idara ya Afya | |
| 3 | Linganisha mtiririko wa gharama za matumizi kwa kila mtumiaji wa huduma ya Afya dhidi ya malengo ya kitaifa? | |
| 4 | Kwa mwaka uliopita, hali ya uchangiaji katika mfuko wa CHF ilikuaje? | |

2. Tathimini ya Mtiririko wa Bajeti ya Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Mtiririko wa Bajeti ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto kama ilivyoainishwa ndani ya CCHP | |

3. Tathimini ya Mtiririko wa Bajeti ya Dawa na Vifaa Tiba

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Mtiririko wa Bajeti ya Dawa na Vifaa tiba kama ilivyoainishwa ndani ya CCHP | |

4. Tathimini ya Hali ya Upatikanaji wa Watumishi wa Afya

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Kuna upungufu wowote kwa kila kada ambao umeainishwa ndani ya CCHP? | |
| 2 | Kiasi gani cha fedha kimetengwa kupunguza upungufu huo? (Kwa kila kada na eneo)? | |
| 3 | Mikakati ipi iliwekwa ili kupunguza masuala ya ukosefu wa maadili kazini? (Rushwa, utoro, wizi wa madawa n.k)? | |

5. Tathimini ya Hali ya Vyoo Safi na Salama

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Kuna vyoo safi na salama katika vituo vya kutolea huduma za afya? | |

6. Tathimini ya Mgawanyo wa Bajeti na Matumizi Halisi

| Na. | Chanzo cha fedha | Makisio ya bajeti | Kiasi kilichopokelewa + salio la nyuma | Kiasi kilichotumika | Bakaa/salio |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LGBG: Mishahara | | | | |
| | Matumizi Mengine | | | | |
| 2 | Mfuko wa Pamoja | | | | |
| 3 | Mfuko wa Dunia | | | | |
| 4 | Serikali Kuu | | | | |
| 5 | Chanzo cha Ndani | | | | |
| 6 | *Uchangiaji wa Pamoja* | | | | |
| | Papo kwa Papo | | | | |
| | NHIF | | | | |
| | CHF | | | | |

7. Tathimini ya Utendaji wa Vyombo vya Usimamizi

| Na. | Eneo la Tathimini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Hali ya Utendaji wa Baraza la Madiwani, Bodi ya Afya na Kamati za Usimamizi wa Vituo? | |
| 3 | Je, kuna masuala ya ukaguzi ambayo hayakupatiwa ufumbuzi? | |

**B. Tathimini ya Mifumo ya Utoaji Huduma za Afya Ngazi ya Vituo vya Kutolea Huduma Vilivypo katika Mradi wa IMPACT**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0 – 49 Isiyoridhisha | | | | | |
| | 50 – 75 Wastani | | | | | |
| | 76 – 100 Nzuri | | | | | |
| | | | | **Idadi ya vituo** | **Asilimia (%)** | |
| | Aina ya kituo | | Hospitali ya wilaya | | | |
| | | | Vituo vya Afya | | | |
| | | | Zahanati | | | |
| | | | **Jumla ya Vituo Chini ya IMPACT** | | | |
| | | | | | | |
| 1 | Tathimini ya Mpango Kazi wa Kituo | 1.1 | Hali ya uwepo wa mpango | | | |
| | | 1.2 | Hali ya uwepo wa kamati ya kuaandaa mpango | | | |
| | | 1.3 | Hali ya uwepo wa muongozo wa upangaji wa mipango | | | |
| | | 1.4 | Hali ya utoaji mafunzo ya uandaaji mpango | | | |
| | | 1.5 | Mchakato wa uidhinishwaji mpango na kamati | | | |
| | | | | | | |
| 2 | Tathimini ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu | 2.1 | Mwaka 2017/18 | | | |
| | | 2.2 | Mwaka 2018/19 | | | |
| | | | | | | |
| 3 | Tathimini ya Utoaji wa Stahiki za Wafanyakazi wa Afya | 3.1 | Malipo ya muda wa ziada | | | |
| | | 3.2 | Malipo ya motisha | | | |
| | | 3.3 | Malipo ya likizo | | | |
| | | 3.4 | Malipo ya sare za kazi | | | |
| | | 3.5 | Malipo ya muda wa dharula | | | |
| | | 3.6 | Posho ya kuwasilisha taarifa ngazi ya Wilaya (Kwa DMO) | | | |
| | | | | | | |
| 4 | Tathimini ya Hali ya Nyumba za Watumishi wa Afya | 4.1 | Hali ya Uwepo wa Nyumba | | | |
| | | 4.2 | Nyumba ambazo hazina ubora kabisa | | | |
| | | 4.3 | Nyumba ambazo zina ubora wa wastani | | | |
| | | 4.4 | Nyumba zenye hali nzuri | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tathimini ya Hali ya Ujenzi na Ukarabati Unaoendelea | 4.5 | Vituo vinavyoendelea na ujenzi | | | |
| | | 4.6 | Vituo vinavyoendelea na ukarabati | | | |
| | | | | | | |
| 5 | Tathimini ya Mbinu za Kubakiza Watumishi Wapya Kazini | 5.1 | Kutoa magodoro kwa watumishi | | | |
| | | 5.2 | Kutoa vitanda kwa watumishi | | | |
| | | 5.3 | Kutoa fedha za kujikimu | | | |
| | | 5.4 | Kutoa motisha nyingine | | | |
| | | | | | | |
| 6 | Tathimini ya Utoaji wa Mafunzo Kazini | 6.1 | Mafunzo ya CTC/PMTCT | | | |
| | | 6.2 | Mafunzo ya MTUHA | | | |
| | | 6.3 | Mafunzo kuhusu huduma za mama na mtoto | | | |
| | | 6.4 | Mafunzo ya huduma za TB | | | |
| | | 6.5 | Mafunzo kuhusu uingizwaji na utunzaji wa takwimu | | | |
| | | | | | | |
| 7 | Tathimini ya Uwepo wa Vifaa vya Mnyororo Baridi | 7.1 | Uwepo wa Jokofu | | | |
| | | 7.2 | Uwepo wa Deli | | | |
| | | | | | | |
| 8 | Tathimini ya Uwepo wa Nishati | 8.1 | Umeme wa TANESCO | | | |
| | | 8.2 | Uwepo wa umeme wa Sola | | | |
| | | 8.3 | Nyingine | | | |
| | | | | | | |
| 9 | Tathimini ya Uwepo wa Vifaa Kinga vya Kuzuia Maambukuzi | 9.1 | Uwepo wa ndoo za kunawia mikono | | | |
| | | 9.2 | Uwepo wa sabuni za maji | | | |
| | | | | | | |
| 10 | Tathimini ya Uwepo wa Vifaa vya Kujikinga na Maambukizi Watumishi | 10.1 | Uwepo wa “gloves” ngumu | | | |
| | | 10.2 | Uwepo wa buti za kufanyia usafi | | | |
| | | 10.3 | Uwepo wa ndoo za kutupia taka zenye rangi tofauti | | | |
| | | 10.4 | Uwepo wa nguo kinga na maski | | | |
| | | 10.5 | Uwepo wa “Chlorine” | | | |
| | | | Uwepo wa mifuko ya taka yenye rangi tofauti | | | |
| | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Tathimini ya Utoaji wa Rufaa kwa Wagonjwa | 11.1 | Hali ya utoaji wa rufaa kwa wagojwa | | | |
| | | 11.2 | Vituo vyenye hadhi ya kuwa na gali la wagonjwa | | | |
| | | 11.3 | Idadi ya magali yaliyopo | | | |
| | | 11.4 | Uwepo wa gali la wagonjwa katika kituo husika | | | |
| 13 | Tathimini ya Uwepo wa Kichomea Taka na Shimo la Kutupia Kondo la Nyuma la Uzazi | 13.1 | Uwepo wa Kichomea taka | | | |
| | | 13.2 | Uwepo wa shimo la kutupia kondo la nyuma la uzazi | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| 14 | Tathimini ya vyanzo vya maji kwenye vituo | 14.1 | Kisima | | | |
| | | 14.2 | Chemchemi | | | |
| | | 14.3 | Bomba | | | |
| | | 14.4 | Maji ya mvua | | | |
| | | 14.5 | Nyingine taja | | | |
| 15 | Tathimini ya Hali ya Vyoo Katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya | 15.1 | Uwepo wa vyoo safi na salama | | | |
| | | 15.2 | Uwepo wa vyoo vya kawaida/wastani | | | |
| | | 15.3 | Uwepo wa vyoo haviko katika hali nzuri | | | |
| | | 15.4 | Uwepo wa vyoo vilivyo zingatia makundi maalumu | | | |

***Tathimni ya Hali ya Upatikanaji wa Vifaa na Vifaa Tiba***

| Vifaa Tiba | Idadi ya Vituo Vyenye Vifaa | Asilimia | | Idadi ya Vituo Vyenye Vifaa Vinavyotumika | Asilimia | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jokofu | | | | | | |
| Mashine za kupima BP | | | | | | |
| Vitakasa vifaa | | | | | | |
| CD4 counting Machine | | | | | | |
| Vitanda | | | | | | |
| Kabati za kuhifadhia dawa | | | | | | |
| Vifaa vingine | | | | | | |

***Tathimini ya Matumizi ya Mifumo ya Kutoa Maoni na kupokea Malalamiko Vituoni***

| Aina ya Mfumo | Idadi ya Vituo | Asilimia | |
|---|---|---|---|
| Sanduku la maoni | | | |
| Kamati ya Afya ya kituo | | | |
| Mikutano ya jamii | | | |
| Njia nyingine | | | |

***Tathimini ya Hali ya Upatikanaji wa Watumishi wa Afya ngazi ya Wilaya***

| Kada | Hospitali ya wilaya | | Kituo cha Afya | | Zahanati | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Mahitaji** | **Waliopo** |
| Daktari | | | | | | | | |
| Tabibu | | | | | | | | |
| Tabibu Msaidizi | | | | | | | | |
| Afisa Muuguzi | | | | | | | | |
| Afisa Muuguzi Msaidizi | | | | | | | | |
| Muuguzi | | | | | | | | |
| Muhudumu wa Afya | | | | | | | | |
| Afisa Afya | | | | | | | | |
| Mtaalamu/ msaidizi wa Dawa | | | | | | | | |
| Mtaalamu/ msaidizi wa Maabara | | | | | | | | |
| Afisa Lishe | | | | | | | | |
| **Jumla** | | | | | | | | |

**Sikika inafanya kazi ya kuhimiza uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha kupitia uwajibikaji jamii na uraghibishi katika ngazi zote za serikali**

Sikika

Nyumba Na.69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika1
Instagram: Sikika1

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania.
Simu: 0262321307
Nukushi: 0262321316